**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA NISHATI (FUNGU 58) KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

---

*[Imetolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

**8 MEI, 2020**

## YALIYOMO


**SEHEMU YA KWANZA** ..... 1
1.0 **UTANGULIZI** ..... 1
1.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ..... 2
1.2 Maelezo na Matokeo ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ..... 2
1.3 Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ..... 10
1.4 Sekta Ndogo ya Gesi Asilia ..... 12
1.5 Umuhimu wa kufanya marejeo ya Mikataba (PSAs) ..... 13
1.6 Hali ya Upatikanaji wa Mafuta Nchini ..... 14
1.7 Hali ya Upatikanaji wa Umeme Nchini ..... 18
1.8 Tathmini ya Miradi ya Umeme Vijijini (REA III) Mzunguko wa Kwanza ..... 20
**SEHEMU YA PILI** ..... 23
2.0 **UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020** ..... 23
2.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli na Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2019/2020 ..... 23
2.2 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa (Fungu 58) Mwaka Wa Fedha 2020/2021 ..... 28
2.2.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ..... 28
2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato ..... 29
2.3.1 Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2020/2021 ..... 29
2.3.2 Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo ..... 29
**SEHEMU YA TATU** ..... 31
3.0 **MAONI NA USHAURI WA KAMATI** ..... 31
4.0 **HITIMISHO** ..... 36

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na Kanuni ya 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Fasili ya 6(9) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati inao wajibu wa kusimamia majukumu na shughuli zinazotekelezwa Wizara ya Nishati. Aidha, majukumu ya Kamati kuhusiana na Uchambuzi wa bajeti ya kila mwaka ya Wizara inazozisimamia yamefafanuliwa katika Fasili ya 7(1)(a).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni, Kamati ilifanya kazi zifuatatazo;

a) Kutembelea na Kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 **[*Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016*]**; na

b) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 **[*Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la Januari, 2016*].**

## 1.1 Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitekeleza matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 kwa kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara ya Nishati (Fungu 58). Ziara hizo zilifanyika katika Mikoa ya Pwani na Dar es Salaam. Lengo la ziara ni kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo chini ya Wizara ya Nishati iliyotengewa Fedha kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, miradi iliyokaguliwa na Kamati yako kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ni kama ifuatavyo;

(i) Miradi ya usambazaji wa gesi asilia majumbani na viwandani mkoa wa Dar es Salaam na Pwani;

(ii) Miradi ya umeme Vijijini REA III Mkoa wa Pwani;

(iii) Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185;

(iv) Kiwanda cha kutengeneza Nyaya na Mashine Umba (Transfoma) cha Africab Mivinjeni Kurasini na Europe Inc Dar es Salaam

## 1.2 Maelezo na Matokeo ya Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maelezo ya miradi pamoja na changamoto ambazo Kamati ilizibaini kwa kila mradi wakati wa ukaguzi wake:

**i. Mradi wa Usambazaji wa Gesi Majumbani Mkoa wa Pwani na Dar Es Salaam**

**Mheshimiwa Spika,** Miradi ya usambazaji wa gesi asilia nchini inatekelezwa na Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya petroli (TPDC). Miradi hii inatekelezwa katika maeneo ambayo tayari kuna miundombinu wezeshi hususani mabomba ya msukumo mkubwa na mdogo ya kusafirisha na kusambaza gesi asilia. Hadi mwezi Februari, 2020 miradi hiyo imeendelea kutekelezwa katika mikoa ya awali ikihusisha mkoa wa Pwani na Dar es Salaam. Uunganishwaji wa wateja wa majumbani na viwandani umeendelea katika mikoa hiyo ambapo wateja hutumia gesi asilia kama nishati mbadala. Sambamba na matumizi haya ya gesi asilia pia gesi hii inatumika katika kuendeshea magari kwa mfumo wa CNG.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwezi Juni 2019 hadi kufikia mwezi Februari 2020 Shirika limejenga miundombinu wezeshi yenye urefu wa kilomita 10.8 yenye uwezo wa kuunganisha nyumba zaidi ya 10,000. Hadi kufikia mwezi Februari 2020 zaidi ya nyumba 385 zimeunganishwa pamoja na "cafeteria" nne za chuo kikuu cha Dar es Salaam. Lengo ni kufikia nyumba za awali zaidi ya 1,385 jijini Dar es Salaam ifikapo mwezi Juni, 2021. Shirika limetenga jumla ya **Shilingi bilioni 3.2** kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea eneo la Mlalakuwa, survey pamoja na eneo la makazi Mikocheni, Dar Es Salaam pamoja na viwanda vya gesi Wilayani Mkuranga na kujionea namna ambavyo gesi imeunganishwa katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kuwepo kwa viwanda vingi maeneo ya Mwanambaya - Mkuranga, Shirika lilitoboa bomba kuu *(hot tapping)* linalotoka Mtwara hadi Dar es Salaam na kutoa toleo kwa ajili ya kuunganisha wateja eneo hilo. Zoezi la utoboaji bomba lililokamilika mwezi Septemba, 2018 limetoa fursa kwa wateja wengi zaidi kuunganishwa na matumizi ya gesi.

**Mheshimiwa Spika,** katika Wilaya hiyo ya Mkuranga, Kamati ilitembelea kiwanda cha *Lodhia Group* eneo la Kisemvule na kuona namna ambavyo mteja ameunganishwa na matumizi ya gesi asilia katika kuendeleza shughuli mbalimbali katika kiwanda hiki.

**Mheshimiwa Spika,** Kiwanda cha chuma cha *Lodhia Group of Industries* kilianza kutumia gesi asilia mwezi Juni, 2019. Kiwanda hiki kinatumia gesi asilia wastani wa futi za ujazo milioni 0.1 - 0.2 kwa siku sawa na makusanyo ya zaidi ya **Shilingi milioni 70** kwa mwezi.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi hii, changamoto iliyobainika ni mahitaji makubwa ya matumizi ya gesi ikilinganishwa na wateja wanaotumia gesi. Aidha, wateja walionesha kiu ya kutaka kuunganishiwa na huduma ya gesi asilia lakini bado utekelezaji wa mradi huu haujafikia wateja wengi.

**Hatahivyo, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Shirika la maendeleo ya Petroli nchini (TPDC) kwa kutoa pesa kwa ajili ya kuunganisha miundombinu ya gesi asilia ambayo imepelekea baadhi ya wateja kufikiwa na huduma ya gesi asilia. Aidha, Kamati inatoa Rai kwa Serikali kupitia TPDC kuongeza kasi ili kufikia wateja wengi zaidi kwa kuwa gesi bado ipo ya kutosha na watuamiaji wengi bado hawajafikiwa.**

**Mheshimiwa Spika,** Uunganishwaji wa gesi asilia majumbani unahitaji kuwekewa mkazo ili uwiane na uharibifu wa mazingira unaosababishwa na matumizi makubwa ya nishati ya mkaa. Utafiti wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii unaonesha kuwa ukataji wa misitu unasababisha kuzalishwa kwa **tani 1,000,000** za mkaa kila mwaka ambapo nusu yake **(tani 500,000)** za mkaa zinatumika jijini Dar es Salaam pekee. **Hivyo ili tuweze kunusuru nchi yetu na janga hili la uharibifu wa mazingira, hatuna budi kuwekeza zaidi na kuruhusu sekta binafsi kushiriki katika miradi ya usambazaji na uunganishaji wa gesi majumbani.**

**ii. Miradi ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA) Mkoa Wa Pwani**

**Mheshimiwa Spika,** Mkoa wa Pwani umekuwa ukinufaika na Miradi ya umeme inayofadhiliwa na Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na kusimamiwa na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO). Miradi ambayo imetekelezwa katika Mkoa wa Pwani mpaka sasa ni REA Awamu ya

kwanza (REA I), Mradi wa Mpito (Interim), REA Awamu ya pili (REA II), Ujazilizi awamu ya kwanza ('Densification' I), REA awamu ya tatu mzunguko wa kwanza na sasa wanatekeleza Mradi kabambe wa *Peri - Urban*.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea wilaya ya Mkuranga kijiji cha kisemvule na kuona utekelezaji wa miradi wa REA awamu ya tatu. Mkandarasi anayetekeleza Mradi huu wenye namba AE/008/2017 - 18/HQ/G/39 Lot 3 ni Ceylex (pvt) Limited. Hata hivyo, mradi huu uko katika hatua za awali za utekelezaji na una thamani ya shilingi **Bilioni 11.64.**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa ukaguzi wa mradi huu changamoto zifuatazo zilibainika;

(a) Mwitikio mdogo wa uunganishwaji wa wateja na huduma ya umeme;
(b) Kasi ndogo ya usambazaji wa umeme;
(c) Maeneo ya vijiji na baadhi ya nyumba kutofikiwa na umeme katika zoezi la kusambaziwa na huduma ya umeme;
(d) Uelewa mdogo wa wananchi juu ya gharama za uunganishwaji na huduma ya umeme;
(e) Wizi wa Mafuta ya Mashine Umba (Transfoma) hivyo kupelekea baadhi kuungua na kukosesha huduma wananchi walio wengi;
(f) Baadhi ya wananchi kuendelea kudai fidia kwa kupitiwa na miundombinu ya umeme licha ya kupewa elimu juu ya kutolipwa fidia.

iii. **Mradi wa Kuzalisha Umeme kwa Kutumia Gesi Asilia wa Kinyerezi I Extension – MW 185**

**Mheshimiwa Spika**, mradi wa *Kinyerezi I Extension* unahusisha uzalishaji wa umeme wa MW 185 kwa kutumia gesi Asilia. Mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Tanzania kwa **asilimia 100** kwa gharama ya **Dola za Marekani milioni 188** sawa na takriban **Shilingi bilioni 435.48**. Ujenzi wa mradi huu ulianza mwezi Novemba, 2016 na ulitarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Disemba, 2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea eneo la Kinyerezi na kujionea hali ya utekelezaji wa mradi huu ambapo kazi zilizokuwa zimetekelezwa ni pamoja na kukamilika kwa utengenezwaji wa mitambo yote minne (4) ya kufua umeme na kuanza kufungwa katika eneo la Mradi; kukamilika kwa upanuzi wa kituo cha kupoza umeme cha *Kinyerezi I Extension*; na kuendelea na upanuzi (*upgrade*) wa njia ya msongo wa **kV 132** kutoka Kinyerezi I hadi kituo cha kupoza umeme cha Gongo la Mboto.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla ujenzi wa mradi ulikua umefikia **asilimia 84**. Aidha, Kamati ilibaini kwamba, kutokana na matatizo ya kifedha yanayo mkabili mkandarasi aliyekuwa anatekeleza mradi huu ilipelekea mradi huu kusimama utekelezaji wake. Hivyo hadi wakati kamati yako inatembelea mradi ulikuwa umesimama utekelezaji wake.

Aidha, Wizara ilitoa taarifa kuwa wako katika hatua za kutafuta mkandarasi mwingine na matarajio ya Wizara ni kukamilisha mradi huu ifikapo mwezi Disemba, 2020.

iv. **Kiwanda cha Europe Inc na Kilimanjaro Cables**

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Kwanza unatekelezwa ipasavyo na kwa haraka, Serikali kupitia Wizara ya Nishati iliwaelekeza wakandarasi wote wanaotekeleza mradi kununua vifaa vyote muhimu vya mradi kutoka kwa wazalishaji wa ndani ya Nchi. Vifaa hivyo ni pamoja na mashine umba *(transfoma),* nyaya na "*cables*". Aidha, kuhusu vifaa ambavyo havizalishwi ndani ya nchi, Wakandarasi waliruhusiwa kuviagiza kutoka nje ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2020, Tanzania ina jumla ya viwanda vitano (5) ambavyo vinafanya uzalishaji wa nyaya zinazotumika kwenye ujenzi wa miradi ya usambazaji wa umeme zenye jumla ya urefu wa kilomita **196,435** za ukubwa mbalimbali kwa Mwaka, wakati mahitaji ya miradi ya REA na TANESCO ni kilometa takiribani **73,654** kwa Mwaka.

**Uwezo wa Uzalishaji wa Nyaya kwa Mwaka**

| Na. | Kiwanda | Mahali kilipo | Uwezo wa Uzalishaji |
|---|---|---|---|
| 1. | East Africa Cables | Vingunguti – DSM | 12,000 |
| 2. | Europe Inc. Industries Ltd | Mikocheni –DSM | 85,435 |
| 3. | Multi Cables Ltd | Chang'ombe - DSM | 25,000 |
| 4. | Kilimanjaro Cables /Africab Ltd | Mivinjeni – DSM | 24,000 |
| 5. | Everwell Cables | Mkuranga – Pwani | 50,000 |
| **Jumla** | | | **196,435** |

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2020, Tanzania ina jumla ya viwanda vitatu (3) ambavyo ni TANELEC, Europe Inc. Industries Ltd na Kilimanjaro Cables (T) Ltd vyenye uwezo wa kuzalisha jumla ya mashine umba (Transfoma) **24,800** za uwezo mbalimbali kwa Mwaka wakati mahitaji ya miradi ya REA na TANESCO ni mashine umba takribani **11,000** kwa Mwaka. Uwezo wa uzalishaji kwa kila kiwanda kwa mwaka ni kama inavyoonekana;

**Uwezo wa Uzalishaji wa Mashine umba kwa Mwaka**

| Na. | Kiwanda | Mahali Kilipo | Uwezo wa Uzalishaji |
|---|---|---|---|
| 1. | TANELEC | Njiro – Arusha | 14,000 |
| 2. | Europe Inc. Industries Ltd | Mikocheni - DSM | 7,200 |
| 3. | Kilimanjaro Cables/ Africab Ltd | Mivinjeni – DSM | 3,600 |
| **Jumla** | | | **24,800** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara katika kiwanda cha European inc pamoja na Kilimanjaro Cables vilivyopo Dar es Salaam na kujionea hali ya uzalishaji wa Mashine-umba (transfoma), nyaya na *cables.* **Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa uamuzi huo unaotoa fursa kwa Makampuni ya ndani kujenga uwezo na kutoa ajira kwa Watanzania. Aidha, Kamati inazipongeza kampuni hizi kwa kuonesha uzalendo wa hali ya juu katika kuitikia wito wa kuwekeza hapa nchini na kuzalisha kwa wingi vifaa hivi muhimu**.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa ziara hiyo Changamoto zifuatazo zilibainika;

a) Wakandarasi wengi pamoja na watoa huduma ya vifaa kutokuwa na uzoefu wa kutumia "letter of credits" ( LC's);
b) Bado hakuna uelewa wa pamoja kwa makampuni ya vifaa katika kutoa huduma kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya REA, hali ambayo imechangia kampuni chache kuweza kupata na kushinda zabuni za kutoa huduma ya kuwauzia wakandarasi vifaa hivi;
c) Madeni ya Kampuni za kuzalisha vifaa kutolipwa kwa wakati na taasisi husika hivyo kufanya uzalishaji kuwa mgumu na vilevile kukwamisha ulipiaji malighafi bandarini kwa wauzaji wa malighafi na gharama nyingine za kiuendeshaji;
d) Baadhi ya malighafi za kutengenezea Mashine-umba (Ambicant Catalyst for XLPE conductor production; GALVANISED Stranded steel wire for ACRS and Arming process) HS-code zake kuhitaji kulipiwa "import duty" hivyo kuongeza gharama za uendeshaji na kuathiri bei ya bidhaa;
e) Mfumo wa ukaguzi bidhaa bandarini kuchukua muda mrefu na hivyo kusababisha malighafi kuchelewa sana kuruhusiwa kutoka bandarini hivyo kuchelewesha upatikanaji wa malighafi na viwanda kulazimika kusimamisha uzalishaji;
f) Ucheleweshaji wa kupatikana kwa cheti cha mazingira kutoka NEMC kwa kampuni ya EUROPE Inc. kumesababisha kutopatikana kibali cha ubora wa kimataifa ISO na hivyo kuleta athari kwenye ushindani wa soko la nje ya nchi.

## 1.3 Maoni ya Jumla Kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

a) Pamoja na mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika usambazaji wa umeme vijijini, Kamati inaona kuwa yapo maeneo mengi ya vijiji na vitongoji yanayohitaji kusambaziwa huduma ya umeme. Kamati inaishauri Serikali kuongeza wigo (scope) kwa wakandarasi ili kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi kufikiwa na nishati ya umeme katika maeneo mbalimbali.

b) Kamati inashauri Serikali kuendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya gharama za uunganishwaji wa huduma ya umeme ili wananchi wafahamu malipo halisi wanayostahili kulipa wanapohitaji kuunganishiwa huduma ya umeme;

c) Serikali iendelee kusimamia na kufuatilia kwa karibu mienendo ya wawekezaji binafsi hususan kwenye eneo la usalama wa wafanyakazi ili kuhakikisha kuwa kanuni za usalama kwa watumishi pamoja na upatikanaji wa maslahi ya watumishi ikiwemo mikataba ya ajira yanazingatiwa;

d) Kufuatia Mkandarasi anaetekeleza mradi wa Kinyerezi I Extension 185MW kushindwa kukamilisha mradi na hivyo kuacha mradi bila kumalizika, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha kuwa "sub-contractors" wote ambao walikuwa wanatoa huduma kwa kampuni hii wanalipwa fedha zao kwa wakati kwani makampuni mengine yana mikopo kwenye mabenki; hivyo jinsi wanavyochelewa kulipwa ndivyo ambavyo riba za mikopo hiyo inavyozidi kupanda na hivyo kuhatarisha uhai wa kampuni hizo;

e) Kwa kuwa hapa nchini ipo gesi ya kutosha, ipo haja kwa TPDC kuongeza kasi ya uungwanishwaji wa wateja wanaohitaji kutumia gesi. Mathalan wakati ambapo katika maeneo ya viwanda yaliyopo

Mkuranga miundombinu ya gesi tayari imefika, lakini uunganishwaji wa wateja haujafikia kiwango cha juu cha mahitaji.

f) Ni vyema kabla Mkandarasi hajapewa mkataba wa kazi ya kupeleka Umeme kwenye Vijiji mbalimbali, kazi ya upembuzi yakinifu kwenye maeneo tajwa ishirikishe wawakilishi wa Wananchi katika ngazi zote ili kuondoa tatizo la Wakandarasi kupewa wigo mdogo wa kazi kinyume na uhalisia wa maeneo/Vijiji husika.

g) Wananchi wengi wa vijijini hawana uelewa mpana wa namna huduma za umeme vijijini zinavyo patikana pamoja na gharama halisi wanazo paswa kulipia ili kuunganishwa huduma ya umeme hali inayosababisha kuwa na muamko mdogo wa kuunganishwa na huduma za umeme. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kutoa elimu ya kina kwa wananchi katika eneo hili.

## 1.4 Sekta Ndogo ya Gesi Asilia

**Mheshimiwa Spika,** Kiasi cha gesi kilichogunduliwa *Gas Initially In Place (GIIP)* katika maeneo ya nchi kavu na baharini kufikia Februari 2020, ni takribani **futi za ujazo Trilioni 57.54**. Kati ya kiasi hicho, gesi iliyogunduliwa nchi kavu (*onshore*) ni **futi za ujazo Trilion 10.46** na kwa upande wa Bahari Kuu (*offshore*) ni **futi za ujazo Trilioni 47.08**. Shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi katika maeneo mbalimbali nchini zinaendelea kufanyika ingawa kwa kipindi kirefu makampuni mengi yalipunguza kasi kwa kuwa yalikuwa yakisubiri kukamilika kwa mapitio ya Mikataba (PSAs).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona kwamba kwakuwa mapitio ya mikataba yamekamilika kwa upande mwingine, TPDC iendelee na shughuli za awali za utafutaji wa mafuta na gesi katika eneo la Eyasi Wembere katika mikoa ya Rukwa, Singida na Manyara ili baadaye maeneo hayo nayo yaendelezwe.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wa taarifa ya sekta ndogo ya gesi, Kamati ilibaini kuwa, Hali ya upatikanaji wa Mafuta, Gesi Asilia na Gesi ya Mitungi nchini imeendelea kuwa nzuri na yenye kuimarika. Ambapo, hadi kufikia mwezi Februari 2020 uwezo wa jumla wa kuhifadhi mafuta katika maghala yaliyo katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ni mita za ujazo 1,127,611. Aidha, miundombinu ya kupokea na kuhifadhi Gesi ya Mitungi (*Liquefied Petroleum Gas* – LPG) katika bandari ya Dar es Salaam na Tanga imefikia uwezo wa kuhifadhi tani 15,600 kwa mara moja. Vilevile, upatikanaji wa Gesi ya Mitungi umeendelea kuwa wa kuridhisha ambapo matumizi yamefikia tani 145,800 kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na hatua hiyo, hali ya mindombinu ya uchakataji, usafirishaji na matumizi ya gesi asilia nchini imeendelea kuwa yakuridhisha. Hadi kufikia mwezi Februari 2020, uwezo wa uzalishaji (uchakataji) wa gesi asilia nchini umefikia futi za ujazo (mmscfd) milioni 210 kwa siku kutoka futi za ujazo (mmscfd) milioni 95 kwa siku mwaka 2015.

### 1.5 Umuhimu wa kufanya marejeo ya Mikataba (PSAs)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yako ilipitia na kufanya uchambuzi kwa kina kuhusu taarifa ya uendelezaji wa mikataba ya gesi asilia nchini ambapo hadi kufikia Januari 2020, mikataba hai ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia iliyopo nchini ni kumi na mbili (12) ambayo inatekelezwa na kampuni za kimataifa nane (8). Mikataba mitatu (3) kati ya hiyo ipo katika hatua za uzalishaji ambayo ni Songo Songo, Mnazi Bay na Kiliwani North; mikataba tisa (9) iko katika hatua ya utafutaji ambayo ni Kitalu Na. 1 na 2, Kitalu Na. 4, Ruvuma, Ruvu, Tanga, Rukwa, Kilosa-Kilombero, Bigwa Rufiji Mafia na Nyuni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa, kwa sasa Shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi katika maeneo mbalimbali nchini zinaendelea kufanyika

ingawa makampuni mengi yamepunguza kasi kwa kuwa yalikuwa yakisubiri kukamilika kwa mapitio ya Mikataba (PSAs) ili yaweze kuhuishiwa leseni zao. Kimsingi mapitio ya mikataba ya utafutaji na uzalishaji mafuta na gesi asilia (PSAs) yanalenga kuhakikisha kuwa Serikali inanufaika ipasavyo kupitia mikataba hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Uwekezaji katika Sekta hii unahitaji mtaji mkubwa, ambapo Serikali nyingi duniani hushirikisha sekta binafsi kwenye utafutaji na uendelezaji wa sekta ya mafuta na gesi asilia. Tanzania inashindana kuvutia uwekezaji na nchi mbalimbali za Afrika kama vile Kenya, Uganda, Angola, Ghana, Mozambique na Nigeria pamoja na nchi za bara la Asia kama vile Qatar, Oman, Trinidad & Tobago na Papua New Guinea. Maamuzi ya Serikali yana mchango mkubwa katika kuvutia au kutokuvutia wawekezaji. Tunaishukuru Serikali kwa kuanza kuhuisha leseni tajwa katika muda muafaka kwakuwa kuchelewa kufanya hivyo kungeleta athari za kupunguza uwekezaji kwa muda katika Sekta hii.

**Mheshimiwa Spika, hata hivyo, pamoja na umuhimu wa kuhuisha leseni husika kwa wakati, madhara makubwa zaidi yanaweza kutokea endapo leseni hizo zitahuishwa bila kufanyika uchambuzi wa kina na wa kutosha katika mikataba (PSAs) iliyopo, umakini mkubwa unahitajika katika zoezi hili la mapitio ya mikataba. Ni matumaini ya Kamati kuwa kazi ya kupitia mikataba (PSAs) itawezesha Serikali na Taifa kwa ujumla kunufaika ipasavyo na rasilimali ya gesi asilia.**

### 1.6 Hali ya Upatikanaji wa Mafuta Nchini

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya jumla ya Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) ni pamoja na kutathmini mahitaji ya Mafuta nchini na kuratibu uagizaji wa Mafuta hayo kwa mfumo wa manunuzi ya pamoja (Bulk procurement System – BPS). Vile vile Wakala amepewa jukumu la kuhakikisha mafuta yanayoletwa nchini yanakidhi mahitaji na ubora

unaotakiwa. Aidha, Taasisi hii imepewa mamlaka ya kuhakikisha mafuta yananunuliwa kwa njia yenye ufanisi (*efficient procurement*) kwa manufaa ya taifa. Pia kuhakikisha uhakika wa usalama wa upatikanaji wa mafuta nchini (*Security of Supply*), na kuiwezesha Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Taasisi mbalimbali za Serikali kukusanya mapato na tozo zitokanazo na mafuta yaliyoagizwa na kwa muda uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya **lita 4,161,067,814.92** za mafuta ya dizeli, petroli, ndege na taa ziliingizwa kwa matumizi ya ndani ya nchi (*local*) na nchi za jirani (*transit*) kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020. Katika kiasi hiki cha mafuta, jumla ya **lita 2,398,969,342.12** sawa na asilimia 58 kilikuwa kwa ajili ya matumizi ya ndani, na **lita 1,762,098,472.80** sawa na asilimia 42 kwa ajili ya nchi za jirani. Ufuatao ni mchanganuo wa kiasi cha Mafuta kilicho agizwa kwa kipindi husika.

| **Mwezi** | **Dizeli (Lita za ujazo)** | **Petroli (Lita za ujazo)** | **Mafuta ya ndege/ Mafuta ya taa(Lita za ujazo)** | **Jumla Kuu** |
|---|---|---|---|---|
| JULAI | 263,073,231.000 | 174,424,348.000 | 34,614,214.000 | 472,111,793.000 |
| AGOSTI | 278,804,029.000 | 178,908,894.000 | 33,002,819.000 | 490,715,742.000 |
| SEPTEMBA | 267,476,245.000 | 155,776,242.000 | 35,887,357.000 | 459,139,844.000 |
| OKTOBA | 340,729,901.000 | 215,889,022.000 | 41,205,525.000 | 597,824,448.000 |
| NOVEMBA | 361,809,665.000 | 230,528,705.000 | 42,452,937.000 | 634,791,307.000 |
| DESEMBA | 321,653,123.000 | 232,376,002.000 | 26,202,176.000 | 580,231,301.000 |
| JANUARI | 303,686,416.000 | 224,310,123.000 | 32,433,934.000 | 560,430,473.000 |
| FEBRUARI | 126,566,339.767 | 213,407,392.817 | 25,849,174.587 | 365,822,907.172 |
| **JUMLA KUU** | **2,263,798,949.767** | **1,625,620,728.817** | **271,648,136.587** | **4,161,067,815.172** |

*Chanzo; **Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa mwaka 2019/2020**.*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilichambua taarifa kuhusu hali ya upatikanaji wa mafuta nchini na kubaini kuwa, kwa kipindi chote cha Julai 2019 hadi Februari 2020 hali ya upatikanaji wa Mafuta nchini ilikuwa nzuri ambapo


nchi ilikuwa na akiba ya Mafuta ya kutosha kwa wastani wa zaidi ya siku 40 kwa kila aina ya Mafuta wakati wote. Hii ni ongezeko la asilimia 55% ikilinganishwa na siku 15 za akiba ya Mafuta zinazotakiwa kwa mujibu wa kanuni.

**Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa BPS (Bulk procurement System) umewezesha kupungua kwa gharama za meli kusubiri kupakua mafuta. Hii imetokana na upangaji na usimamizi mzuri wa uletaji meli za mafuta (*laycan*) ambao umepelekea muda wa meli kusubiri kupungua kutoka wastani wa siku 45 kwa siku za nyuma hadi wastani wa siku 5 kwasasa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa, kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020 gharama za Meli kusubiri imepungua kwa **asilimia 18.4** ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2018/2019. Ufuatao ni mchanganuo wa gharama husika;

| **MONTH** | **SPM** | | **KOJ1** | | **AVERAGE** | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **MONTH** | **Y2018/19** | **Y2019/20** | **Y2018/19** | **Y2019/20** | **Y2018** | **Y2019** |
| **Jul** | 1.6321 | 1.2882 | 4.4243 | 1.3612 | 3.0448 | 1.3182 |
| **Aug** | 1.7682 | 1.4277 | 4.9680 | 1.2314 | 3.1017 | 1.5236 |
| **Sep** | 2.2745 | 1.8200 | 4.5162 | 1.1303 | 3.2114 | 1.6820 |
| **Oct** | 1.4084 | 1.3747 | 2.7909 | 1.2254 | 1.9559 | 1.3149 |
| **Nov** | 1.8162 | 1.9164 | 1.4815 | 1.1363 | 1.6679 | 1.6037 |
| **Dec** | 1.7824 | 2.3169 | 1.8874 | 2.7974 | 1.8295 | 2.5263 |
| **Jan** | 2.8816 | 1.4651 | 1.9527 | 4.8693 | 2.4942 | 2.9472 |
| **Feb** | 1.4179 | 1.6519 | 3.0135.7539 | 4 | 2.0990 | 2.7334 |
| **OVERALL** | **1.8883** | **1.6951** | **3.1013** | **2.3459** | **2.4028** | **1.9610** |

18.4%




*Chanzo;* ***Taarifa ya Utekelezaji wa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa mwaka 2019/20.***

**Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na hali ya upatikanaji wa mafuta nchini pamoja na usimamizi mzuri wa uagizaji wa mafuta unaofanywa na Wizara kupitia Wakala wa uagizaji wa mafuta kwa pamoja (PBPA) kwa kushirikiana na mamlaka nyingine. Ni matumaini ya Kamati kuwa Wakala wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja utaendelea kusimamia sekta ya mafuta kwa ufanisi kwa manufaa ya uchumi wa nchi yetu.**

Aidha, Kamati ina matumaini kuwa Wakala utaendelea kushirikiana na Wadau wengine kwa lengo la kuendelea kuimarisha mfumo wa uagizaji wa Mafuta nchini hususan katika kipindi hiki ambapo Ulimwengu unakabiliwa na changamoto kubwa ya Ugonjwa wa homa ya Mapafu (COVID -19); changamoto ambayo Taasisi mbalimbali za Utafiti za Kimataifa kama IMF, World Bank, UNECA, na Fitch Solutions zinatabiri kutokea kwa mdororo wa uchumi ulimwenguni utakaoathiri shughuli za kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Tayari Ulimwengu umeanza kushuhudia Sekta za Usafiri wa Anga na Utalii kusimama, biashara na uzalishaji viwandani kushuka na

hivyo kushuka kwa kiasi kikubwa kwa matumizi ya mafuta. Kufuatia kushuka kwa matumizi ya mafuta ulimwenguni tumeshuhudia vilevile katika siku za hivi karibuni bei ya mafuta kwenye soko la kimataifa kushuka kwa kiwango kikubwa ambacho hakijawahi kushuhudiwa. **Hivyo basi kufuatia mkanganyiko huu na mwenendo usiotabirika wa soko la mafuta ulimwenguni, ipo haja kwa nchi yetu kuweka mikakati thabiti ya kuhakikisha nchi inakuwa na akiba ya mafuta ya kutosha wakati wote. Aidha, Serikali itumie mwanya huu wa mdororo wa bei ya mafuta ulimwenguni kuzungumza na nchi rafiki zinazozalisha mafuta ili kama nchi tuweze kupata mafuta kwa masharti nafuu sasa, na kupitia TPDC tuweze kuanzisha hifadhi ya mafuta ya kimkakati kwa ajili ya kuhami uchumi wetu kwa siku zijazo.**

### 1.7 Hali ya Upatikanaji wa Umeme Nchini

**Mheshimiwa Spika**, Shirika la Umeme nchini (TANESCO) linaendesha mfumo uliounganishwa wa Gridi ya Taifa wenye mitambo ya kufua umeme kwa kutumia maji, gesi asilia na mafuta.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yako ilifanya uchambuzi kuhusu taarifa ya hali ya upatikanaji umeme nchini na kubaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2020 uwezo wa mitambo ya kufua umeme iliyounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa ulikuwa **Megawati 1,565.72** ambapo Megawati 573.70 (36.64%) zinatokana na vyanzo vya nguvu ya maji, Megawati 892.72 (57.02%) ni vyanzo vya gesi asilia, Megawati 88.80 (5.67%) zinatokana na Mafuta na Megawati 10.50 (0.67%) zinazalishwa kutokana na mabaki ya mimea na mazao (Biomass). Uwezo wa mitambo hiyo unajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO ambayo huchangia **asilimia 86.50** na mitambo ya wazalishaji binafsi (IPPs/SPPs) ambayo huchangia **asilimia 13.50**. Aidha, Shirika linamiliki mitambo ambayo haijaunganishwa katika mfumo wa gridi ya Taifa yenye uwezo

wa kufua **Megawati 36.598** na hivyo kufanya jumla ya uwezo wa mitambo ya kufua umeme nchini kufikia **Megawati 1,602.318**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati yako ilibaini kuwa mahitaji ya juu ya umeme katika mfumo wa gridi ya Taifa yameendelea kukua kwa kasi ambapo kwa mwezi Februari, 2020 pekee mahitaji yameongezeka kutoka **Megawati 1,125.36** zilizofikiwa tarehe 07 Februari, 2020 saa 3 usiku na kufikia **Megawati 1,151.66** zilizofikiwa tarehe 27 Februari, 2020 saa 3 usiku. Hili ni sawa na ongezeko la **asilimia 3.14** ukilinganisha na **Megawati 1,116.58** zilizokuwa zimefikiwa mwaka 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, TANESCO pia hununua umeme kutoka kwa wazalishaji wadogo (SPPs) ndani ya nchi ambao ni: Mwenga **MW 4**; TPC **MW 9**; TANWAT **MW 1.5**; Yovi **MW 0.95**; Tulila **MW 5**; Darakuta **MW 0.32**; Andoya **MW 0.5**; na Matembwe **MW 0.59**. Aidha, TANESCO ina mikataba ya kununua umeme kutoka nje ya nchi (imports) ambapo **MW 17** ni kutoka Uganda kwa ajili ya Mkoa wa Kagera; **MW 1** ni kutoka Kenya kwa ajili ya Wilaya ya Longido; na **MW 5** ni kutoka Zambia kwa ajili ya Mkoa wa Rukwa. **Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada kubwa zinazofanyika katika kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na umeme wa kutosha, uhakika na unaotabirika wakati wote kutoka katika vyanzo mchanganyiko kwa kushirikisha wazalishaji wadogo (Small Power Projects – SPP). Aidha, ili kulinda uwekezaji ambao tayari wazalishaji wadogo wa umeme wameufanya na hivyo kuweza kuhudumia zaidi ya wateja 100,000 hapa nchini na vilevile kuendelea kujenga imani kwa wawekezaji kuwa mazingira ya ufanyaji biashara hapa nchini yanatabirika, Kamati inaona ipo haja kwa Serikali kuharakisha mchakato wa kutafuta suluhu ya mkanganyiko wa bei ya kuuzia umeme unaozalishwa na wazalishaji wadogo.**

1.8 **Tathmini ya Miradi ya Umeme Vijijini (REA III) Mzunguko wa Kwanza**

**Mheshimiwa Spika**, Jumla ya vijiji vilivyokuwa vimefikiwa na umeme hadi kufikia **31.12.2015** ni **2,018.** Aidha, Jumla ya vijiji vilivyofikiwa na umeme Tanzania Bara hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020 ni 9,112**.** Jumla ya vijiji vitakavyofikiwa na umeme Tanzania Bara (miradi ya **Off-grid(REA & Private), REA III – Round I, Densification I na REA II pamoja na miradi ambayo inatekelezwa na TANESCO)** itakapokamilika mwezi Juni 2020 ni: **10,446.** Jumla ya vijiji vitakavyobaki bila umeme ifikapo 01.07.2020 ni: **1,822.** Aidha, Jumla ya vijiji Tanzania Bara kwa mujibu wa TAMISEMI 2015 ni: **12,268.** Jumla ya taasisi zilizofikiwa na umeme hadi 31.12.2015 ni **4,036** na Jumla ya taasisi zilizofikiwa na umeme hadi 29.02.2020 ni **11,377.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yako ilichambua taarifa ya Utekelezaji wa miradi ya REA na kufanya tathmini ya namna ya utekelezaji wake ambapo Mradi wa REA awamu ya tatu unatekelezwa katika mikoa 25 ya Tanzania Bara. Mradi umegawanya katika mafungu 29 (29 Lots) ambayo yanatekelezwa na jumla ya wakandarasi 16 ambapo kati yao, wakandarasi 11 ni wazawa na wakandarasi 5 ni kutoka nje ya nchi. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2020.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa pamoja na changamoto ndogo ndogo za Wananchi wengi kuhitaji umeme, hali ya utekelezaji wa mradi wa umeme vijijini kwa wastani unaridhisha.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia tarehe 26.03.2020 jumla ya **TZS 457,477,112,939.87 (VAT Inclusive)** sawa na **asilimia 53** za gharama nzima ya mradi kwa upande wa fedha za ndani na **USD 80,912,192.86 (VAT Inclusive)** sawa na **asilimia 71** za gharama nzima ya mradi kwa

upande wa fedha za kigeni zimelipwa kwa wakandarasi kwa ajili ya kazi za mradi pamoja na ununuzi wa vifaa.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 31.12.2019 Wakala ulifanya tathmini ya wakandarasi wanaotekeleza mradi wa kusambaza umeme vijijini awamu ya tatu mzunguko wa kwanza (REA III Round I) na kubaini kuwa jumla ya mikataba **22** kati ya **29** sawa na **asilimia 75.9** ilikua inatekelezwa vizuri juu ya malengo. Aidha, mikataba **5** kati ya **29** ilikuwa katika wastani na **mikataba 2** ilikua inatekelezwa chini ya malengo. Kufuatia kubainika kwa mikataba 2 ambayo utekelezaji wake ulikuwa chini ya malengo, hatua za kimkataba zilichukuliwa ambapo wakandarasi wanaoitekeleza waliandikiwa barua (Notice of Default) tarehe 10.01.2020 yenye Kumb. Na.: AG 143/171/09/Vol. II/85 ikieleza nia ya Muajiri kutaka kuvunja mkataba na kuwapatia kipindi cha siku 14 kufanya marekebisho ya mapungufu yote na kuhakikisha mikataba inakamilika kwa wakati. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kuchukua hatua hizo. Hatua hizo zimeyafanya Makampuni kuongeza kasi katika utendaji wake.**

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na kazi nzuri inayoendelea kufanywa na Wakala wa Umeme vijijini (REA) zipo changamoto kadhaa zinazohitaji kuboreshwa. Maeneo hayo ni pamoja na mwamko mdogo wa wananchi kuunganishwa na huduma ya umeme katika baadhi ya maeneo ambayo tayari miundombinu imefika.

**Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaona ipo haja ya wakandarasi kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi hii, hatahivyo, Serikali inapaswa kuendelea kuweka nguvu ya kiusimamizi na ufuatiliaji wa wakandarasi wanaotekeleza miradi hii kuhakikisha kuwa miradi hii inakamilika kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa kulingana na matakwa ya mikataba.**

**Aidha, iko haja ya Serikali wa kupanua wigo (scope) ya utekelezaji wa miradi hii ili kuwafikia Watanzania wengi kwa wakati mfupi.**

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti kwa kuzingatia mambo makuu matatu ambayo ni:-

a) Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2019/2020;

b) Hali ya upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina na;

c) Uzingatiaji wa maoni na ushauri uliotolewa na Kamati ya Nishati na Madini wakati huo.

### 2.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Maduhuli na Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2019/2020

#### a) Makusanyo ya Maduhuli kwa mwaka wa Fedha 2019/2020;

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Nishati ilipangiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 602.05.** Kati ya makusanyo hayo, jumla ya **Shilingi bilioni 602.04** zilitarajiwa kukusanywa kupitia shughuli za mafuta na gesi asilia na **Shilingi 12,000,000.00** kupitia shughuli za utawala. Mapato hayo yanatokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo: Shughuli za TPDC za utafiti wa mafuta; Mauzo ya gesi asilia; na Mauzo ya Nyaraka za Zabuni.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwezi Julai 2019 hadi Februari 2020 jumla ya **Shilingi bilioni 377.15** zilikusanywa kutokana na shughuli za mafuta na gesi asilia zilizoratibiwa na TPDC. Kamati ilibaini kuwa Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 89.5** ya lengo la makusanyo ya **Shilingi bilioni 421.36** kwa kipindi hicho. Aidha, **Kamati inatoa rai kwa Wizara kuendelea na jitihada za kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo vya mafuta na gesi asilia.**

b) **Hali ya upatikanaji wa fedha kutoka Hazina;**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka 2019/2020, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliidhinisha Bajeti ya Jumla ya **Shilingi 2,142,793,309,000** kwa Wizara ya Nishati. Kati ya Fedha hizo, Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ni **Shilingi 2,116,454,000,000** sawa na **asilimia 98.8** ya bajeti yote ya Wizara. Bajeti ya Fedha za ndani iliyotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 1,956,372,000,000** sawa na **asilimia 92.4** ya Bajeti yote ya Maendeleo. **Shilingi 160,084,000,000** sawa na **asilimia 7.6** ni fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kwa Mwaka 2019/2020 ni **Shilingi 26,339,309,000** sawa na **asilimia 1.2** ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) na **Shilingi 11,313,488,000** kwa ajili ya kulipa mishahara (P.E) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2019 hadi Februari 2020 Fedha zilizopokelewa kwa bajeti ya Wizara ya Nishati ni **Shilingi bilioni 686.63** sawa na **asilimia 68.4** ya lengo la miezi minane (8). Kati ya Fedha hizo zilizopokelewa, **Shilingi bilioni 9.91** ni fedha za matumizi mengineyo (O.C) ambayo ni sawa na **asilimia 98.9** ya lengo na **Shilingi bilioni 6.5** ni mishahara sawa na **asilimia 86.3** ya lengo.

Aidha, **Shilingi bilioni 670.20** ni za miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 67.9** ya lengo la fedha za maendeleo. Fedha za ndani zilizopokelewa ni **Shilingi bilioni 572.34** sawa na **asilimia 65.8** ya lengo la fedha za ndani na **Shilingi bilioni 97.88** sawa na **asilimia 83.9** ya lengo la fedha za nje. Kamati ilibaini kuwa Fedha hizo zimetokana na kazi ambazo tayari zimekamilika na hati za madai *(certifícates and invoices)* kuwasilishwa na kuhakikiwa.

Kwa kazi ambazo zinaendelea, Kamati ilielezwa kuwa madai yake hayajawasilishwa kwa ajili ya malipo, na kwamba pindi kazi husika zikikamilika na hati za madai husika kuwasilishwa; madai hayo yatalipwa. Aidha, baadhi ya miradi hupokea fedha za ndani na za nje kulingana na wakandarasi wanavyowasilisha madai *(certifícates and invoices)*, na baadhi ya miradi hupokea fedha za nje moja kwa moja (*direct to Project funds*) ambazo taarifa zake huingizwa (kuhesabiwa) katika hesabu za Wizara mwisho wa mwaka husika.

**Ni Rai ya Kamati kuwa mara baada ya madai husika kuwasilishwa, Fedha za Miradi ya Maendeleo zitatolewa kwa wakati.**

**MUHTASARI WA FEDHA ZILIZOPOKELEWA KWA MWAKA 2019/2020**

**HADI KUFIKIA MWISHONI MWA MWEZI FEBRUARI 2020**

| Na | Matumizi | Bajeti iliyopitishwa kwa Mwaka 2019/20 | Fedha zilizotakiwa kutolewa mpaka mwezi Februari 2020 | Fedha zilizotolewa mpaka Februari Mwaka 2019/20 | % ya fedha zilizot olew a |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Matumizi Mengineyo OC | 15,025,821,000 | 10,017,214,000 | 9,914,412,412 | 98.9 |
| 2 | Mishahara (P.E) | 11,313,488,000 | 7,542,325,500 | 6,510,721,670 | 86.3 |
| | **Jumla Ndogo** | **26,339,309,000** | **17,559,539,500** | **16,425,134,082** | **93.5** |
| 3 | Fedha za Ndani | 1,956,372,000,000 | 869,498,666,600 | 572,318,312,891 | 65.8 |
| 4 | Fedha za Nje | 160,082,000,000 | 116,712,133,300 | 97,883,725,361 | 83.9 |
| | **Jumla Ndogo** | **2,116,454,000,000** | **986,210,799,900** | **670,202,038,252** | **67.9** |
| | **JUMLA KUU** | **2,142,793,309,000** | **1,003,770,339,400** | **686,627,172,334** | **68.4** |

***Chanzo; Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara ya Nishati (Fungu 58) kwa mwaka wa Fedha 2019/2020***

c) **Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Bajeti ya Mwaka 2019/2020 Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo, kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Toleo la Januari, 2016 inayoelezea majukumu ya Kamati ya kusimamia na kufuatilia utendaji kazi wa shughuli za Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa, sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na baadhi unaendelea

kufanyiwa kazi zaidi na Serikali. Maoni ambayo kamati inaamini ni muhimu na yanahitaji kufanyiwa kazi zaidi ni yafuatayo:-

i. **Miundombinu wezeshi ya mradi wa umeme wa mto Rufiji (Nyerere hydropower)** hasa barabara, madaraja na makalavati ni vema ikawa imara na ya kudumu na kuweza kupitika wakati wote ili kuhakikisha kuwa ujenzi wa mradi unatekelezwa bila vikwazo.

ii. **Mfumo wa gawio la mapato yatokanayo na Mafuta na Gesi** - Upo umuhimu wa Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya mafuta na Gesi ya mwaka 2015 kuangaliwa upya ili pamoja na mambo mengine ibadili mfumo wa kuigawia TPDC fedha za mfuko wa Gesi Asilia na Mafuta kwa kutegemea uchangiaji wa Pato la Taifa (GDP) kwa asilimia 3.

iii. **Ulipaji Fidia wananchi** - Serikali ilipe fidia kwa wakati kwa wananchi wote wanaotoa maeneo yao kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

    **Aidha, Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kulipa fidia ya takribani kiasi cha Shilingi bilioni 5.2 kwa wananchi waliopisha utekelezaji wa mradi wa gesi Asilia (LNG) mkoani Lindi. Hakika kilio chao kilikuwa cha muda mrefu na sasa Serikali imetekeleza kiu ya wananchi hawa kwa wakati muafaka.**

**Mheshimiwa Spika, Ni Rai ya Kamati kuwa Wizara itaendelea kufanyia kazi maoni na ushauri unaotolewa na Kamati.**

## 2.2 Uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa (Fungu 58) Mwaka Wa Fedha 2020/2021

### 2.2.1 Mapitio ya Malengo ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Nishati inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wake. Kulingana na Mpango Mkakati huo Wizara ina malengo makuu sita (6) ambayo ni:

i) Kuongeza uzalishaji na kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme;
ii) Kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika matumizi mbalimbali ya nishati;
iii) Kuimarisha shughuli za utafiti na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia;
iv) Kuboresha rasilimali za Wizara ili kutoa huduma bora za nishati;
v) Kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Kuzuia Rushwa; na
vi) Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI sehemu za kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa waathirika.

**Mheshimiwa Spika, pamoja na malengo hayo Wizara inapaswa kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na Taasisi zake katika kusimamia Sekta ya Nishati ikiwemo kuendelea kuelimisha umma na kuboresha mawasiliano kati ya Wizara na wadau mbalimbali kuhusu masuala ya nishati.**

## 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

### 2.3.1 Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2020/2021

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka 2020/2021, Wizara ya Nishati (Fungu 58) inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi 2,488,289,499,000** ikilinganishwa na **Shilingi 2,142,793,309,000** zilizotengwa kwa Mwaka 2019/2020 sawa na ongezeko la **asilimia 16.1**.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kwa Mwaka 2020/2021 ni **Shilingi 28,399,590,000** sawa na **asilimia 1.1** ya bajeti yote ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 15,025,821,000** zitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C) na **Shilingi 13,373,769,000** ni kwa ajili ya mishahara (P.E) ya watumishi wa Wizara na Taasisi zilizopo chini yake.

### 2.3.2 Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika mwaka 2020/2021 unakadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 2,459,889,909,000** ambazo ni sawa na **asilimia 98.9** ya bajeti yote ya Wizara. Bajeti ya fedha za ndani zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 1,967,689,292,000** sawa na **asilimia 80** ya Bajeti yote ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa Kiasi kikubwa cha fedha za ndani za maendeleo kimeelekezwa katika miradi ya kielelezo na kimkakati ambayo ni: Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere, MW 2,115; Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu; Mradi wa Kuzalisha Umeme wa Kinyerezi I Extension MW 185; na Miradi ya Ruhudji, Rumakali, Singida - Arusha - Namanga, Iringa - Mbeya - Sumbawanga - Kigoma na LNG, EACOP. Aidha, Bajeti ya Fedha za Nje inayopendekezwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni **Shilingi 492,200,617,000** sawa na **asilimia 20** ya Bajeti yote ya Maendeleo.

**Muhtasari wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka 2020/2021**

| A: FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA | | |
|---|---|---|
| **MAELEZO** | **BAJETI** | **ASILIMIA (%) YA BAJETI YOTE** |
| Mishahara (P.E) | 13,373,769,000.00 | |
| Matumizi Mengineyo (O.C) | 15,025,821,000.00 | |
| **Jumla Fedha za Matumizi ya Kawaida** | **28,399,590,000.00** | **1.1 %** |
| **B: FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO** | | |
| Fedha za Ndani | 1,967,689,292,000.00 | |
| Fedha za Nje | 492,200,617,000.00 | |
| **Jumla Fedha Za Maendeleo** | **2,459,889,909,000.00** | **98.9 %** |
| **JUMLA KUU** | **2,488,289,499,000.00** | **100%** |

***Chanzo;*** *Maelezo ya Randama kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka 2019/2020*

Aidha, kwa upande wa makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2020/2021, Wizara inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 160,622,137,324.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 160,601,745,679** zitakusanywa kupitia shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia; na **Shilingi 20,391,645** zitakusanywa kupitia shughuli za utawala. **Kamati inatoa angalizo kwa Serikali kuwa upo uwezekano mkubwa wa kuwepo kwa mdororo wa shughuli za uwekezaji ulimwenguni kutokana na uwepo wa janga la COVID-19; hali ambayo inaweza kuathiri makisio ya makusanyo yaliyowekwa. Kwa muktadha huu, Kamati inaishauri Serikali kufuatilia kwa karibu hali ya uwekezaji inavyoendelea ulimwenguni ili kuweza kufanya mapitio ya haraka kwenye mipango iliyowekwa.**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 **MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kutekeleza majukumu yake ya kikanuni ambayo ni ukaguzi wa miradi ya maendeleo na uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali: -

### 3.1 Utekelezaji wa Mradi wa Julius Nyerere - MW 2,115

Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji katika Bonde la Mto Rufiji (Julius Nyerere - MW 2,115) una umuhimu wa kimkakati kwa uchumi wa taifa letu, **Na kwakuwa** katika mwaka 2019/20 utekelezaji wake ulijielekeza katika ujenzi wa miundombinu wezeshi; **Na kwamba** kwa mwaka 2020/2021 mradi unaingia katika hatua muhimu sana ya utekelezaji ikiwemo kuanza kwa ujenzi wa bwawa (main dam and spillways), ujenzi wa njia kuu za kupitisha maji (tunnels), ujenzi wa kituo cha kuzalishia umeme (Power House) na ujenzi wa kituo cha kusafirisha umeme (Switch yard). Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha kuwa inaongeza usimamizi, na kuhakikisha Fedha za uendelezaji wa mradi zinapatikana kwa wakati kama zilivyotengwa na kuidhinishwa na Bunge.

### 3.2 **Utekelezaji wa Mradi wa Kinyerezi I Extension**

Kamati ilibaini kuwa mkandarasi anayetekeleza mradi wa *Kinyerezi I Extension* 185MW ameshindwa kutekeleza majukumu yake ya kimkataba na kuuacha mradi bila kumalizika, kutokana na changamoto hiyo Kamati inatoa rai kwa Serikali kuhakikisha mkandarasi mwingine wa kumalizia mradi anapatikana kwa haraka. **Aidha** Serikali ifanye jitihada za makusudi

kuhakikisha “sub-contractors” wote ambao walikuwa wanatoa huduma kwa mkandarasi wa awali wanalipwa fedha zao kwa wakati ili kuwaepusha na hatari ya kufilisika kutokana na kupanda kwa riba za mikopo waliyochukua kwenye mabenki.

### 3.3 **Viwanda vya Kuzalisha Vifaa vya Umeme Nchini.**

Uwezo wa uzalishaji wa viwanda vilivyopo unazidi mahitaji ya soko nchini na kwakuwa hata uzalishaji kwa ajili ya soko la ndani unafanyika bila ya wazalishaji kupata takwimu halisi za mahitaji kwa mwaka hivyo kushindwa kukadiria vyema mahitaji ya malighafi na kujipanga kwenye mizunguko ya uzalishaji, **Hivyo basi** Kamati inaishauri Serikali kuvisaidia viwanda vyetu kutafuta masoko nje ya nchi kwa kuweka mkakati mahsusi wa kuzishirikisha ofisi zetu za ubalozi kwenye ukanda wa Afrika mashariki na SADC; kufanya hivi sio tu kutawezesha bidhaa za viwanda hivi kupenya kwenye masoko ya nchi hizo bali pia itaongeza mapato ya kikodi kwa nchi yetu. **Vilevile,** Kamati inashauri REA na TANESCO kutangaza mapema mahitaji yao ya mwaka ya Mashine-umba ili kuwezesha viwanda hivi kujipanga na kuzalisha kwa ufanisi.

**Sambamba na hili,** baadhi ya malighafi muhimu za kutengenezea Mashine-umba (Ambicant Catalyst, na GALVANISED Stranded steel wire) HS code zake uhitaji kulipiwa ‘import duty’ hivyo kuongeza gharama za uendeshaji na kuathiri bei ya bidhaa; **Na kwakuwa** mfumo wa ukaguzi bidhaa bandarini huchukua muda mrefu hivyo kusababisha malighafi kuchelewa, na viwanda kulazimika kusimamisha uzalishaji; **NA** kutopatikana kwa cheti cha mazingira kutoka NEMC kumesababisha kutopatikana kibali cha ubora wa kimataifa ISO kwa kampuni ya Europe Inc Industries Ltd na hivyo kuathiri ushindani wa soko la nje ya nchi, **Kamati inaishauri** Serikali iangalie namna bora ya kushughulikia changamoto hizi kwa

kushirikiana na mamlaka zingine za Serikali ili vibali na bidhaa ziweze kupatikana kwa wakati na bila vikwazo.

### 3.4 Bei ya Umeme Unaozalishwa na Wazalishaji Wadogo (SPPs/ Minigrids)

Serikali ilifanya uamuzi mahsusi wa kuwashirikisha wazalishaji wadogo wa umeme (Small Power Projects – SPP) kuwekeza nchini ili kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na umeme wa uhakika kutoka katika vyanzo mchanganyiko; **Na kwakuwa** wazalishaji wadogo waliitikia wito wa Serikali kuwekeza, Hivyo basi ili kulinda uwekezaji ambao tayari umefanywa na wazalishaji wadogo ambao wanahudumia zaidi ya wateja 100,000 hapa nchini; **Na vilevile** ili kuendelea kujenga imani kwa wawekezaji kuwa mazingira ya ufanyaji biashara hapa nchini yanatabirika, **Kamati inaona ipo haja** kwa Serikali kuharakisha mchakato wa kutafuta suluhu ya mkanganyiko uliopo sasa wa bei ya kuuzia umeme unaozalishwa na wazalishaji wadogo.

### 3.5 Kuvutia Uwekezaji Katika Sekta ya Nishati

Uandaaji wa miongozo ya kutangaza miradi inayotekelezwa kwa kutumia vyanzo vya Makaa ya Mawe, Jua, na Upepo kwa njia ya ushindani ulikamilika tangu Oktoba 2018, na zabuni za miradi hiyo kutangazwa Novemba 2018 kwaajili ya kuzalisha MW 600 za makaa ya Mawe, MW 150 za Umeme wa Jua; na MW 200 za umeme wa Upepo, Kamati inasisitiza kuwa ni muhimu uchambuzi wa zabuni hizo ambao umechukua muda mrefu ukakamilika haraka ili ujenzi wa miradi hii uweze kuanza mwezi Oktoba 2020 na kukamilika mwezi Desemba 2021 kama ilivyokusudiwa.

### 3.6 Matumizi ya Gesi Asilia Majumbani

Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya petroli (TPDC) imeanza kutekeleza miradi ya usambazaji wa gesi asilia katika maeneo ambayo tayari kuna miundombinu wezeshi; **na kwakuwa** hadi

kufikia mwezi **Februari 2020** tayari miundombinu yenye urefu wa **kilomita 10.8** imejengwa ikiwa na uwezo wa kuunganisha zaidi ya nyumba 10,000; **kwa mtazamo wa Kamati** kasi ya uunganishwaji gesi asilia majumbani hailingani na uhitaji uliopo, wala kasi ya uharibifu wa mazingira unaosababishwa na matumizi makubwa ya nishati ya mkaa nchini; **Hivyo basi** ili tuweze kunusuru nchi yetu na janga hili la uharibifu wa mazingira hatuna budi kuwekeza zaidi na kuruhusu sekta binafsi kushiriki katika miradi ya usambazaji na uunganishaji wa gesi majumbani.

### 3.7 Tahadhari ya Athari za COVID -19, Kuhusiana na Upatikanaji na Matumizi ya Mafuta Nchini;

Dunia inakabiliwa na changamoto kubwa ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu (COVID -19); changamoto ambayo Taasisi mbalimbali za Utafiti za Kimataifa kama IMF, World Bank, UNECA, na Fitch Solutions zimetoa angalizo la uwezekano wa kutokea mdororo wa uchumi duniani, **Na kwakuwa** tayari dunia imeanza kushuhudi Sekta za Usafiri wa Anga na Utalii zikisimama, biashara na uzalishaji viwandani kushuka na hivyo kushuka kwa kiasi kikubwa kwa matumizi ya mafuta; na bei ya mafuta kwenye soko la kimataifa kuporomoka kwa kiwango kikubwa ambacho hakijawahi kushuhudiwa. Kufuatia mkanganyiko huu na mwenendo usiotabirika wa soko la mafuta ulimwenguni, ipo haja kwa nchi yetu kuweka mikakati thabiti ya kuhakikisha nchi inakuwa na akiba ya mafuta ya kutosha wakati wote; **Na halikadhalika** kutafakari namna bora ya kutekeleza miradi ya REA ambayo utekelezaji wake unategemea chanzo cha tozo kutoka kwenye mafuta yanayotumika nchini.

### 3.8 Kasi ya uunganishwaji wa wateja na huduma ya umeme;

Serikali kufanya tathmini kuhusu kasi ya kuunganisha wateja waliolengwa kuunganishwa na huduma ya umeme kwakuwa makisio ya uunganishwaji wa wateja yanatakiwa kuwiana na hali ya uzalishaji wa umeme.

### 3.9 Utaratibu wa uagizaji wa Liquefied Petroleum Gas (LPG)

Matumizi ya Gesi ya LPG hapa nchini yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku. Hatahivyo gharama ya upatikanaji wake ni kubwa, hali inayosababisha bei kwa mtumiaji wa mwisho kuwa juu. Kamati inatambua kuwa kupitia agizo la Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. John Pombe Magufuli wakati akizindua hifadhi ya gesi ya kampuni ya Taifa Gas, Serikali kupitia PBPA ilianza mchakato wa kufanya majadiliano na EWURA, WMA, TPA, TRA na Wafanyabiashara wa LPG nchini ili kuweka utaratibu bora utakaokuwa na manufaa kwa pande zote. Kamati inashauri Serikali kuharakisha majadiliano hayo na kuja na mapendekezo yatakayowezesha gesi ya LPG kupatikana nchini kwa mfumo wenye tija kwa watumiaji na taifa kwaujumla.

### 3.10 Usimamizi wa Wakandarasi wanaotekeleza miradi ya REA;

Bado zipo changamoto kadhaa katika miradi ya REA, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha usimamizi wa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya REA ili miradi hiyo ikamilike kwa wakati kama ilivyo katika matakwa ya mkataba; Aidha, ipo haja Serikali kuongeza wigo (scope) ya utekelezaji wa miradi hii kwani maeneo yanayoainishwa ni madogo ukilinganisha na uhitaji.

## 3.11 **Udhibiti wa upotevu wa Mafuta katika miundombinu ya kupokelea mafuta;**

Ili kuendelea kudhibiti upotevu wa Mafuta katika miundombinu ya upokeaji wa Mafuta, Kamati inashauri Kampuni zote za Mafuta zinazomiliki Hifadhi za Mafuta kufunga *flowmeters* kwa kila njia ya kupokelea Mafuta. Aidha, Serikali kupitia wakala zake wasimamie zoezi hili ili kuhakikisha linatekelezwa kikamilifu na kwa wakati.

## 3.12 **Wigo wa kutoa huduma kwa wananchi wa mijini na vijijini;**

Serikali iielekeze TANESCO kubuni njia bora zaidi ya kusogeza huduma zake karibu na wananchi bila kutumia gharama kubwa kwani wateja wengi hususan wa sehemu za vijijini wanakosa huduma kwakuwa maeneo yao hayajafikiwa na ofisi za TANESCO.

## 4.0 **HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge, kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuliongoza Bunge hili Tukufu. Mungu awajalie afya njema, hekima na busara katika kutekeleza wajibu huu mkubwa tuliowakabidhi**.**

Aidha, Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa Waziri wa Nishati Mhe. Dkt Medard Matogolo Kalemani, (Mb), Mhe. Subira Khamis Mgalu, (Mb)- Naibu Waziri wa Nishati pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Eng. Zena Ahmed Said kwa kusimamia vema shughuli za Wizara na kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati yetu wakati wote.

Kwa namna ya pekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, kwa weledi na umahiri waliouonesha wakati wote wa kutekeleza majukumu ya kamati. Kwa heshima kubwa naomba majina yao katika orodha ifuatayo yaingizwe kwenye kumbukumbu rasmi za Bunge:-

1. Mhe. Dunstan Luka Kitandula, Mb - **MWENYEKITI**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb – **M/MWENYEKITI**
3. Mhe. Hamida Mohamed Abdallah, Mb
4. Mhe. Catherine Valentine Magige, Mb
5. Mhe. Hamoud Abuu Jumaa, Mb
6. Mhe. Vedastus Mathayo Manyinyi, Mb
7. Mhe. Jesca David Kishoa, Mb
8. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb
9. Mhe. Ussi Salum Pondeza, Mb
10. Mhe. Mwantakaje Haji Juma, Mb
11. Mhe. Maryam Salum Msabaha, Mb
12. Mhe. Wilfred Muganyizi Lwakatare, Mb
13. Mhe. Kiza Hussein Mayeye, Mb
14. Mhe. Mohamed Juma Khatib, Mb
15. Mhe. Bahati Ali Abeid, Mb
16. Mhe. Msukuma Joseph Kasheku, Mb
17. Mhe. Yosepher Ferdinandi Komba, Mb
18. Mhe. James Kinyasi Millya, Mb
19. Mhe. Lameck Okambo Airo, Mb
20. Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb
21. Mhe. Zubeda Hassan Sakuru, Mb
22. Mhe Ally Mohamed Keissy, Mb
23. Mhe. John Wegesa Heche, Mb
24. Mhe. Frank George Mwakajoka, Mb

25. Mhe. Abdallah Ally Mtolea, Mb

**Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndg. Ndg. Felister Mgonja na Ndg. Herman Berege na msaidizi wa Kamati Ndg. Grace Mwenye kwa uratibu mzuri wa shughuli zote za Kamati na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema haya sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 58** Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja ambayo ni **Shilingi 2,488,289,499,000.**

**Mheshimiwa Spika,** naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Dunstan Luka Kitandula, (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI**
8 Mei, 2020